



Mamlaka ya Udhubiti Usafiri Ardhini

**NJIA ZA DALADALA ZILIZOIDHINISHWA ILI KUFIKISHA
HUDUMA MASOKO YA WAMACHINGA DAR ES SALAAM**

Kufuatia maagizo ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoyatoa kwa Mamlaka ya Udhubiti Usafiri Ardhini tarehe 25 Januari, 2022 Ikulu Jijini Dar es Salaam, kuhakikisha huduma ya usafiri inafika kwenye masoko ya Serikali yaliyotengwa kwa ajili ya Wamachinga Jijini Dar es Salaam, Mamlaka inapenda kuwajulisha kuwa imesitisha utoaji wa leseni za usafirishaji kwa daladala kuanzia tarehe 27 Januari, 2022 **kwa baadhi ya njia** ili kutoa kipaumbele kwa njia zinazokwenda au kupita kwenye masoko hayo.

Hivyo, Mamlaka inawashauri wasafirishaji kuchagua njia zilizo orodheshwa katika jedwali kwa mujibu wa maelekezo haya wakati wa kuhuisha au kuomba leseni mpya ili kuepuka usumbufu.

Kwa maelezo zaidi piga simu namba 0758 80 77 31

Imetolewa na;

Mamlaka ya Udhubiti Usafiri Ardhini (LATRA)

28 Januari, 2022